



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA

Tovuti: www.hlpc.go.tz



TANGAZO

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI (INTERNSHIP)

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukuwa nafasi hii kuwajulisha Wataalamu wote wanaotarajia kufanya maombi ya utarajali (internship) kwa ngazi ya Shahada (Bachelor Degree) mwezi **Aprili 2023** kuwa dirisha la maombi ya utarajali litafunguliwa rasmi tarehe **16 Machi 2023 saa 4:00 Asubuhi** na litafungwa **17 Machi 2023 saa 9:30 alasiri**

Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo;

1. Maombi ya utarajali yatafanyika mtandaoni kupitia mfumo wa usajili (hprs.moh.go.tz)
2. Waombaji wote wawe wameshafanya maombi ya usajili wa awali (Provision Registration) kwenye mfumo wa usajili ikiwemo kulipia ada ya Usajili kabla ya dirisha la usajili kufungwa
3. Kila kituo cha utarajali kina idadi ya Watarajali takiwa, hivyo kila mtarajali atatakiwa kuwahi nafasi katika kituo anachokihitaji kabla ya nafasi kujaa
4. Kabla ya dirisha kufungwa, mfumo utamruhusu mtarajali kubadili kituo alichomba kwenda kituo kingine kama kituo anachokihitaji kitakuwa na nafasi (hakijajaa). Baada ya dirisha kufungwa hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha kituo cha utarajali.
5. Kikao cha Watarajali watakaopangiwa vituo vya utarajali kitafanyika siku ya Alhamisi ya tarehe **30 Machi 2023 saa 2:30 Asubuhi** jijini Dodoma. Pia kikao hicho kitahusisha kuchukua nyaraka za utarajali.
6. Video fupi inayoelekeza jinsi ya kufanya maombi ya Utarajali inapatikana katika karasa za mitandao ya kijamii ya Baraza (Instagram: [hlpc_tanzania](https://www.instagram.com/hlpc_tanzania) | Twitter: [@hlpc_tanzania](https://twitter.com/hlpc_tanzania) | Facebook: Baraza la Wataalam Maabara)

Upatapo tangazo hili mtaarifu mwenzako.

Imetolewa na ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara

